JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI NA. 12- 2019/2020**

**DHIDI YA**

**CLASSIC FM RADIO**

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA ZA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA UTANGAZAJI WA REDIO NA TELEVISHENI), 2018**

## 1.0 Utangulizi

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, ilitoa leseni ya huduma ya Matangazo (Matangazo ya Redio) kwa kituo cha **Classic FM Radio** kwa ajili ya kutoa huduma ya utangazaji.

1.2 Kwa mujibu wa Kanuni Na. 45 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018, kituo cho chote chenye leseni ya kurusha matangazo ya Redio au Televisheni kitakachokiuka Kanuni hizi kinaweza kuchukuliwa hatua stahiki za kisheria.

1.3 Tarehe 20/02/2020 kati ya saa 07.00 mchana na saa 10.00 Jioni kituo cha **Classic FM Radio** kinatuhumiwa kukiuka Kanuni na maadili ya utangazaji kwa kuendesha kipindi kijulikanacho kwa jina la **Pepeta.** Kipindi hicho kilikuwa na maudhui yenye lugha isiyo na staha na yenye kuudhi na kudhalilisha waumini wa dini ya Kiislamu na jamii kwa ujumla.

1.4 Watangazaji wa kipindi cha **Pepeta** walisikika, wakiendesha kipindi kwa kutumia lugha isiyo na staha ambayo haikuzingatia Weledi, Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari, walipokuwa wakitoa maneno ya kejeli kwa kutumia lugha ya Kiarabu na yenye kuashiria kuikashifu dini ya Kiislam.

1.5 Watangazaji walisikika wakitumia lugha hiyo ya kejeli isiyo na staha walipokuwa wakizungumza maneno yafuatayo: ***..yaanini mtu akukoseshe raha anakulipia kodi hapa mjini, anakulisha wewe ndugu yangu, mnachangia bwana mjini, kitu gani ndugu yangu***

***mwenye macho kama tochi ya sungu sungu...eheheeeee.....na kwa nini ubabaishwe na mtu mwenye* sura kama Alif-Laam-Meem...**

## 2.0 Kanuni zilizokiukwa

Kitendo cha kuendesha kipindi chenye maudhui yenye lugha isiyo na staha na yenye kuashiria kukashifu, Kituo cha **Classic FM Radio** kimekiuka Kanuni Na.11 (1) (c) na 29 (c) & (e) za Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018, ambazo zinasomeka kama ifuatavyo;-

*11.-(1) A licensee shall ensure that the programme and its presentation: -*

*(c) observes good taste and decency;*
*29. A content services licensee shall;*
*(c) Take particular care to avoid blasphemy and take into account cultural and religious sensitivities;*
*(e) Avoid using improper language, pronunciations, or mixing of languages.*

## 3.0 Wito wa kufika mbele ya Kamati ya Maudhui

Tarehe 03 Machi 2020, Kamati ya Maudhui iliuandikia Uongozi wa **Classic FM Radio,** wito wa kufika mbele ya Kamati kutoa utetezi wake kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

Tarehe 13 Machi, 2020, saa 05:00 asubuhi, Uongozi wa **Classic FM Radio** ukiongozwa na Bw. Emmanuel Ngalapa, Mkuu wa vipindi wa **Classic FM Radio** aliyeambatana na Bw Fungo Emmanuel, Afisa Sheria wa Africa Media Group ambayo inamiliki Kituo cha **Classic FM Radio**, ulifika mbele ya Kamati ya Maudhui kwa ajili ya kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

## 4.0 CLASSIC FM RADIO kusomewa Shitaka

Kamati ya Maudhui iliusomea Uongozi wa **Classic FM Radio** shitaka lao na kuhakiki kwa pamoja kipindi kinacho lalamikiwa. Kisha Uongozi huo ulipewa fursa ya kujitetea kwanini hatua za kisheria zisichukuliwe dhidi ya **Classic FM Radio** kwa kukiuka Kanuni za Maudhui ya utangazaji wa Redio na Televisheni.

## 5.0 Maelezo ya Utetezi wa CLASSIC FM RADIO

5.1 Katika utetezi wao wa maandishi, Uongozi wa **Classic FM Radio** ulikana tuhuma zilizotolewa juu yao na kudai kuwa chombo chao cha habari hakijakiuka Kanuni za Huduma za Utangazaji zilizoanishwa katika wito huo.

5.2 Aidha, Uongozi huo ulisema kuwa hakukuwa na kiashiria cho chote cha kuikashifu dini ya Kiislam, labda tu tafsiri ya maneno. Aliongeza kuwa Kituo chao kimekuwa kikizingatia misingi ya utangazaji ikiwamo kutokashifu wala kutoa viashiria vya kukashifu imani ya Dini.

5.3 Uliendelea kusema kuwa neno lililotamkwa **Alif-Laam-Meem** ni neno la Kiarabu hivyo kutaja neno hilo si kukashifu imani ya Kiislam na kuongeza kuwa hata Mhubiri maarufu wa dini ya Kiislam Dr. Zakir Abdul Karim ambaye naye amejaribu kuelezea maana ya neno hilo alidai kuwa kuna baadhi ya wahubiri hulihusisha na Mwenyezi Mungu huku wengine wanasema maneno hayo yanaongeza vionjo na hayana maana ye yote.

5.4 Lakini Dr Karimu yeye anasema neno hilo lina maana ya herufi kama A,B,C za lugha ya kiarabu, na hivyo hata wao Classic FM wanakubaliana na mhubiri hyo kuwa alimaanisha kitu kingine na si kukashifu dini au imani fulani.

5.5 Waliendelea kudai kuwa sio kila neno la kiarabu linaakisi kukashifu imani fulani, kwani hata maneno mengi ya Kiswahili yana asili ya Kiarabu, hivyo kuna uhusiano mkubwa kati ya Kiswahli na Kiarabu.

5.6 Pia walidai kuwa kipindi chao kinachohusishwa na tuhuma hizo ni cha muziki wa mwambao, yaani **taarabu** na hata neno hilo limetoholewa kutoka lugha ya Kiarabu yaani **tarab.**

5.7 Uongozi wa **Classic FM Radio** uliongeza hoja yao ya utetezi kwa kunukuu kesi ya ***Hamisi Rajab Dibagula Vs Republic 2003 AHRL A274*** ambapo mshatakiwa alituhumiwa kwa kutamka maneno ya kibaguzi yenye kudhihaki dini ya Kikristo kwa kusema kuwa *"Yesu sio Mungu"*, na kukutwa na hatia. Lakini alipokata rufaa Mahakama ya Rufaa katika hukumu yake ilisisitiza umuhimu wa uvumilivu wa kidini/kiimani.

5.8 Pia walidai kuwa tuhuma za kutumia lugha isiyo na staha si kweli kwa sababu kipindi husika kinahusu muziki wa mwambwao ambao una ujumbe wa mipasho. Aidha walisema kuwa katika muziki wa taarabu mipasho siyo matusi au lugha mbaya kwani ni namna ya muziki unavyotakiwa uwe.

Pamoja na utetezi wao wa maandishi, **Classic FM Radio** waliendelea kueleza yafuatayo;

5.9 Bw Ngalapa alisema mtangazaji aliyetamka neno hilo alimaanisha herufi za Kiarabu na si kukashifu imani fulani.

5.10 Aliendelea kudai kuwa huwa inakuwa vigumu kujua mtu watakayemwalika atatatumia maneno gani katika kuelezea mada fulani, kwa kuwa humpatia mwalikwa mada lakini maneno ya kuongea huchagua mwenyewe.

5.11 Bw Fungo alidai kuwa mneno ya mipasho ni namna ya undeshaji wa kipindi ambapo mtangazaji au mgeni mwalikwa huwa anachambua muziki wa taarabu.

5.12 Katika kujumuisha utetezi wao, Bw. Fungo aliendelea kusisitiza kuwa hawajakiuka kanuni ye yote au kukashifu Imani ya mtu, lakini wanabaki kuwa wanyenyekevu na wasikivu kwa Kamati ya Maudhui juu ya tuhuma zinazowakabili.

## 6.0 Tathmini ya Kamati

6.1 Kamati ya Maudhui imebaini kuwa **CLASSIC FM RADIO** imefanya kosa la kutokuwa waangalifu na makini katika kutumia lugha na hivyo kutangaza maudhui yenye ukakasi na yasiyozingatia weledi kwa mujibu wa Kanuni Na. 29 (c) na (e) ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018

6.2 Kamati ya Maudhui imeona kuwa utetezi wa **Classic FM Radio** kuwa neno **Alif-Laam-Meem** ni neno la Kiarabu tu na hivyo kutaja neno hilo si kukashifu imani ya Kislam, na kumnukuu Mhubiri maarufu wa dini ya Kiislam ***Dr. Zakir Abdul Karim*** kuwa neno hilo halina maana kwa wengine na kwa baadhi ni vionjo tu na kwamba wao wanalichukulia kama herufi za kiarabu tu. Utetezi huu hauna nguvu kwa sababu hata huyo Mhubiri waliyemnukuu na katika utetezi wao kwenye aya ya pili wamekiri kuwa huyo mhubiri anasema neno hilo kwa wengine wanasema lina ishara ya Mwenyezi Mungu. Hivyo wao hawaoni kuwa kwa watu wanaoamini kuwa neno hilo lina ishara ya Mwenyezi Mungu kuwa wamekashifiwa au wamekwazwa?

6.3 Aidha, Kamati imeona kuwa neno **Alif-Laam-Meem** linaweza likatafsiriwa kwa namna ya kuhusisha na imani ya Kiislamu kwa sababu kwa tafsiri nyingine ya neno hilo ni ***Sura ya Kwanza ya Juzuu.*** Juzuu ni kitabu kitakatifu cha kufundishia Dini ya Kiislamu.

6.4 Pia, Kamati imeona kuwa utetezi wa **Classic FM Radio** unaorejea hukumu ya Mahakama ya Rufani kwenye kesi ya **Hamisi Rajabu Dibagula** kuwa kila mtu ana wajibu wa kuwa na uvumilivu wa kiimani kama hukumu inavyosema, utetezi huo hauna msingi kwa sababu hakuna kipimo cha uvumilivu.

6.5 Hata hivyo, ni dhahiri kuwa watu hawawezi kuwa na kiwango sawa cha uvumilivu kwa jambo linalogusa imani kwa sababu jambo hilo linapokuwa linarushwa hewani na vyombo vya habari huwafikia watu wengi, wenye maoni na tafsiri tofauti juu ya jambo husika ukilinganisha na jambo kama hilo linapotokea katika mihadhara ya kidini ambako ndiko ***Bwana Dibagula*** alitoa matamshi yaliyomfanya kushitakiwa na ndipo Mahakama ya Rufaa katika hukumu yake iliwataka watu kuwa na uvumilivu wa kidini kwa sababu kwenye mihadhara ni watu walioko katika mhadhara huo pekee ndio watapata ujumbe husika. Ujumbe huo huo ukitangazwa kwenye vyombo vya habari unakuwa na madhara makubwa kwa jamii

6.6 Hali kadhalika Kamati imebaini kwamba utetezi wa **Classic FM Radio wa** kutaka kuwepo na uvumilivu kidogo tu wa kidini hauna msingi kwa sababu mambo yanayogusa imani ni nyeti na yakipuuzwa au kuachwa kwa kisingizio cha kutaka kuenzi uvumilivu wa kidini yanaweza kuchochea chuki na hivyo kusababisha madhara makubwa kwa jamii.

6.7 Vile vile, Kamati imeona kuwa utetezi kwamba muziki wa tarabu una mahadhi ya mipasho na hivyo utumiaji wa lugha isiyo na staha kuwa ndiyo halali yake si sahihi kwa sababu hata katika muktadha wa kipindi cha taarabu unaweka mipasho, lakini mipasho hiyo lazima iwe na mipaka.

6.8 Kamati imeona kwamba Mtangazaji wa **Clasic FM Radio** hawezi kufanya kipindi cha mipasho kinachoruka hewani kwenye Kituo hicho akitumia maneno ya mipasho yanayofanana na yale atakayozungumza mtangazaji huyo huyo anapokuwa mshereheshaji (MC) kwenye kumbi za starehe au sherehe yoyote ile. Hivyo, linapokuja suala la kurusha maudhui kwa njia ya redio, televisheni au mitandao ya kijamii, Mtangazaji anatakiwa kuwa na Weledi pamoja na kuzingatia Maadili, Sheria na Kanuni za utangazaji.

## 7.0 Ushauri wa Kamati kwa Classic FM Radio.

7.1 Kamati ina lengo la kuimarisha tasnia ya habari na utangazaji na kuwa haina nia ya kubana ubunifu wa watangazaji wa vipindi na muziki ya taarabu, bali inawataka wanahabari kuzingatia weledi Sheria na Kanuni na maadili ya uandishi wa habari. Na pia kutofautisha maneno ya mipasho wanayotumia wawapo vijiweni au kwenye kumbi za starehe na maneno yatakayotumika wanaporusha maudhui kwa njia ya Redio, Televisheni na mitandao ya kijamii.

7.2 Kamati inatambua kuwa suala la utangazaji linahitaji watu wenye ubunifu wa hali ya juu, elimu bora, maadili na weledi katika tasnia ya Habari, hivyo **Classic FM Radio** inatakiwa kuwaelimisha watendaji wake ili wawe makini wanapozungumzia jambo ambalo linaweza kutafsiriwa vibaya.

7.3 Hata hivyo, kutokana na kosa lililobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa **Classic FM Radio** kuweka usimamizi mzuri wa habari na vipindi vyao na wageni wanaowaalika studioni ili wasiweze kutamka maeno ambayo yatatafsiriwa vibaya. Hatua hiyo itaiwezesha **Classic FM Radio** kuepuka kuvunja sheria na Kanuni za nchi.

## 8.0 Uamuzi wa Kamati

Baada ya kusikiliza na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi yaliyotolewa na Uongozi wa **Classic FM Radio**, Kamati ya Maudhui imejiridhisha pasi na shaka kuwa kituo cha **Classic FM Radio** kimekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018.

**Hivyo basi**, kwa mujibu wa Kifungu cha 28 (1) (b) na (d) cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172, Marejeo ya Mwaka 2017, Kamati ya Maudhui inaamua kutoa adhabu zifuatazo kwa Kituo cha **Classic FM Radio;**

1. Kulipa faini ya **Shilingi Milioni moja (TZS. 1,000,000.00)** tu kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa mujibu wa Kanuni Na. 45. ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018;

2. Wanapewa Onyo kali.

Uamuzi huu umetolewa na kusomwa Dar es Salaam leo ya tarehe **17** mwezi **Machi** mwaka **2020**

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal - FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia leo.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Bwana Joseph Method Mapunda**

..........................................................................

**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

**PAMOJA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MAUDHUI WAFUATAO;**

1. **Bwana Abdul Ramadhani Ngarawa**..................................
2. **Bwana Derek Kaitira Murusuri**......................................
3. **Bwana Jacob Gregory Tesha**.........................................